## ,FUNZO LA 8

1. Je, Mungu alitayarisha nchi kwa malaika au kwa Shetani na mapepo wake?
-La.

2. Mungu alitayarishia nani nchi?
-Mungu alitutayarishia nchi sisi wanadamu.

3. Kwa kila kitu alichoumba Mungu, cha muhimu zaidi ni nini?
-Wanadamu.

4. Kwa sababu wanadamu walikuwa wa muhimu zaidi ya kila kitu ambacho Mungu aliumba, je Mungu aliamua kutuumba vipi?
-Mungu aliamua kutuumba kwa mfano wake.

5. Ni sehemu ipi ya wanadamu iliyoumbwa kwa mfano wa Mungu?
-Akili, hisia na mapenzi yetu.

6. Mungu anataka tufanye nini na akili yetu?
-Mungu anatutaka tufikirie kilicho kizuri.
-Mungu anatutaka tumfikirie yeye.

7. Kwa nini Mungu akatupatia hisia?
-Ili tumpende Mungu.

8. Mungu anataka tufanye nini na mapenzi yetu?
-Mungu anatutaka tuchague kile kilicho kizuri.
-Mungu anataka tumchague yeye.



9. Hapo mwanzo, Mungu aliwaumba watu wangapi?
-Mwanamume mmoja na mwanamke mmoja pekee.

10. Jina la mwanamume wa kwanza ni lipi?
-Adamu.

11. Baada ya Mungu kumuumba Adamu, alimfanyia nini?
-Mungu alimpa Adamu mamlaka juu ya nchi.

12. Hapo mwanzo, maisha yalikuwa manna gani?
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na hasira.
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na chuki.
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na uovu.
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na kifo.

13. Nani aliyekuwa akitazama wakati Mungu aliumba dunia kamilifu?
-Malaika wa Mungu, Shetani, na mapepo wake.

14. Je, Shetani na mapepo wake walifurahi kwa sababu Mungu aliumba dunia kamilifu?
-La.

-Je, Mungu alimaliza kuumba mbingu na nchi?
-Ndiyo.

Tusome Mwanzo 2:1

1-Hivyo ndivyo mbingu na dunia zilivyokamilika pamoja na vitu vyote vilivyomo.

-Mungu alimaliza kuumba vitu vyote.
-Mungu alimaliza kufanya kazi yote aliyoipanga kuifanya.

-Wakati mwingine wanadamu wanaanzisha kazi lakini hawaimalizi.

-Wakati mwingine wanaume huanza kujenga nyumba lakini hawaimalizi.

-Wakati mwingine wanawake huanza kufinyanga chungu lakini hawakimalizi.

-Wakati mwingine watu hawamalizi kwa sababu kazi ni ngumu sana.

-Wakati mwingine watu hawamalizi kwa sababu wamesimamishwa na mtu mwingine.

-Mungu si kama wanadamu.

-Mungu akianza kazi, hasimamishi kwa sababu kazi ni ngumu.
-Mungu akianza kazi, hasimamishi kwa sababu amesimamishwa na mtu.

-Mungu akianza kazi, huikamilishaa kazi hiyo.

-Kwa nini Mungu humilisha kazi ambayo ameanzisha?



-Kwa sababu Mungu habadiliki.

-Kwa sababu hakuna chochote kinachoweza kumzuia Mungu kumaliza kazi yake.

-Wakati Mungu anapoanza kazi yake, je wanadamu wanaweza kuisimamisha?
-La.
-Wakati Mungu anapoanza kazi yake, je Shetani na mapepo wanaweza kuisimamisha?
-La.

-Mungu akitoa ahadi kuwa atafanya jambo fulani, ni lazima atekeleze.

-Wacha tusome kile Mungu alifanya baada ya kuumba mbingu na nchi:

Tusome Mwanzo 2:2-3

2-Siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyofanya; siku hiyo ya saba Mungu akapumzika baada ya kazi yake yote aliyofanya.
3-Mungu akaibariki siku ya saba na kuitakasa, kwa sababu siku hiyo Mungu alipumzika baada ya kazi yake yote ya kuumba.

-Kwa nini Mungu alipumzika siku ya saba?
-Je, Mungu alikuwa amechoka?
-La.

-Kwa nini Mungu hakuwa amechoka baada ya kuumba vitu vyote?

-Kwa sababu Mungu hachoki.
-Kwa sababu nguvu za Mungu hazina mwisho.

-Kwa nini Mungu alipumzika siku ya saba?

-Kwa sababu Mungu alikuwa amemaliza kuumba kila kitu alichokuwa amekipanga kuumba.

-Mungu aliumba vitu vyote kwa siku ngapi?
-Siku sita pekee.

-Inachukuwa siku ngapi kukamilisha kujenga nyumba?
-Pengine zaidi ya miezi mitatu.

-Tazama vitu vyote alivyoumba Mungu kwa siku sita pekee.

-Mungu pekee ndiye angeweza kuumba mbingu na nchi kwa siku sita pekee.

Tusome Mwanzo 2:4b & 6

4-Siku ile BWANA Mungu alipoziumba mbingu na dunia,
6-Hata hivyo, maji yalitoka ardhini yakainywesha ardhi yote.

-Mungu alipoiumba nchi mwanzo, hakukuwa na mvua.



-Kama hatukuwa na mvua hapo mwanzo, je Mungu aliinyunyizia aje nchi maji?

-Mungu alinyunyizia nchi maji kutokana na ukungu uliotoka ardhini.

Tusome Mwanzo 2:8

8-Kisha BWANA Mungu akapanda bustani huko Edeni, upande wa mashariki, na humo akamweka huyo mwanamume aliyemuumba.

-Hapo Mwanzo, Mungu alipanda bustani ya kupendeza.

-Jina ya bustani iliyopandwa na Mungu ni?
-Bustani ya Edeni.

-Mungu alimpandia nani bustani ya Edeni?
-Adamu.

-Kwa nini Mungu alimpandia Adamu bustani ya Edeni?
-Kwa sababu Mungu alimpenda Adamu sana.

-Mungu alipopanda bustani, alimweka Adamu kwenye bustani hiyo.

-Je, Mungu alimwuliza Adamu kama angemweka kwenye bustani ya Edeni?
-La.
-Kwa nini Mungu hakumwuliza Adamu kama angemweka kwenye bustani ya Edeni?

-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu, Adamu alikuwa wa Mungu.

-Kwa sababu Mungu aliwaumba wanadamu wote, wanadamu wote ni wa nani?
-Wanadamu wote ni wa Mungu.

-Kwa vile Mungu ndiye muumba wa vitu vyote, vitu hivi vyote ni vya nani?
-Vitu vyote ni vya Mungu.

-Katikati ya bustani ya Edeni, Mungu alipanda miti miwili maalum.

Tusome Mwanzo 2:9b

9-Katikati ya bustani hiyo kulikuwa na mti wa uhai na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

-Jina la mti wa kwanza ambao Mungu alipanda katikati ya bustani ya Edeni ni lipi?

-Mti wa Uzima.

-Kwa nini Mungu aliupanda mti wa uzima katikati ya bustani ya Edeni?

-Mungu alimtaka Adamu ale matunda ya mti huo ili aishi milele.



-Mungu hakumlazimisha Adamu kula matunda ya mti wa uzima.

-Mungu alimtaka Adamu ajichagulie.
-Mungu alimtaka Adamu achague kula matunda ya mti wa uzima.

-Mungu alimtaka Adamu kuchagua uzima.

-Jina la mti wa pili ambao Mungu aliupanda katikati ya bustani ya Edeni ni lipi?

-Mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

-Kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya, Mungu alimpa Adamu amri.

Tusome Mwanzo 2:16-17a

16-BWANA Mungu alimwamuru huyo mwanamume, “Waweza kula matunda ya mti wowote katika bustani;
17-walakini matunda ya mti wa ujuzi wa wema na mabaya usile.”

-Kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya, ni amri ipi Mungu alimpa Adamu?

-Mungu alimwamuru Adamu asile matunda ya mti huo.

-Mungu anajua kile kilicho chema na kile kibaya.

-Mungu anajua kile chema ni chema na kile kiovu ni kiovu.

-Hapo mwanzo Adamu alijua kile kilicho chema pekee.
-Hapo mwanzo Adamu hakujua uovu wowote.

-Wacha tusome kile Mungu alisema kitamtendekea Adamu akila kutoka kwa mti wa ujuzi wa wema na mabaya:

Tusome Mwanzo 2:17b

17-BWANA Mungu akamwambia Adamu, "Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo, hakika utakufa."

-Kama Adamu angekula tunda la mti wa ujuzi wa wema na mabaya, nini kingemfanyikia?

-Adamu angekufa.
-Kifo ni nini?

-Watu wengi husema kuwa kuna kifo kimoja tu.
-Mungu anasema kuna vifo vitatu.

-Kifo cha kwanza ni kutenganishwa na Mungu.

-Kwa nini kutenganishwa na Mungu ni kifo?

-Kwa sababu Mungu pekee ndiye anayepeana uhai.
-Kwa sababu uhai wote unatoka kwa Mungu.

-Lusifa alitenda dhambi, na alitenganishwa na Mungu.



-Ikiwa Adamu hangemtii Mungu, angetenganishwa na Mungu.

-Kifo cha pili ni kutenganishwa kwa roho kutoka kwa mwili.

-Hiki ndicho kifo ambacho watu wengi wanajua.
-Ikiwa Adamu hangemtii Mungu, mwili wake ungekufa.

-Kifo cha tatu ni kutenganishwa milele kwenye ziwa la moto wa milele.

-Ikiwa Adamu hangemtii Mungu, nafsi yake ingeenda kwenye ziwa la moto wa milele.

-Ikiwa Adamu hangemtii Mungu, angetengwa kutoka kwa Mungu, mwili wake ungekufa, na nafsi yake ingeenda kwenye ziwa la moto wa milele.

-Kwa nini Mungu alimwagiza Adamu asile matunda kutoka kwa mti wa ujuzi wa wema na mabaya?

-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu.
-Kwa sababu Adamu alikuwa wa Mungu.

-Ikiwa mtu atatengeneza jembe, si jembe hilo ni la mwanaume huyo?
-Ndiyo.

-Mwanamke akitengeneza kikapu, si kikapu hicho ni cha mwanamke aliyekitengeneza?
-Ndiyo.

-Ikiwa mtoto atatengeza mwanasesere, si huyo mwanasesere hiyo ni wa mtoto aliyeitengeneza?
-Ndiyo.

-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu, Adamu alikuwa wa Mungu.

-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu, Mungu angeweza kumwagiza Adamu.

-Je, ilikuwa vyema kwa Mungu kumwagiza Adamu?
-Ndiyo.

-Kwa nini ilikuwa vyema kwa Mungu kumwagiza Adamu?
-Kwa sababu Mungu ana hekima kuliko Adamu.

-Je, mzee ana hekima nyingi kuliko mvulana mdogo?
-Ndiyo.

-Je, mama mkongwe ana hekima nyingi kuliko msichana mdogo?
-Ndiyo.

-Je, kuna umuhimu wowote kwa wavulana wadogo kusikiliza mawaidha ya wazee?
-Ndiyo.

-Kuna umuhimu wowote kwa wasichana wadogo kusikiliza mawaidha kutoka kina mama wazee?
-Ndiyo.



-Kwa sababu Mungu alikuwa na hekima zaidi kushinda Adamu, ilikuwa jambo la muhimu Adamu kumsikiliza Mungu.

-Kwa nini Mungu alimtaka Adamu amsikilize?

-Kwa sababu Mungu ana hekima zaidi ya Adamu.
-Kwa sababu Mungu alijua kile chema kwa Adamu.

-Kwa sababu Mungu alijua kile kibaya kwa Adamu.
-Kwa sababu Mungu alitaka kumlinda Adamu.

-Wazee wanajua yale yalio mema na mabaya kwa vijana.

-Wanawake wazee wanajua yalio mema na mabaya kwa wasichana.

-Ni nani aliyejua yalio mema na mabaya kwa Adamu?
-Mungu.

-Nani anayejua yalio mema kwa watu wote?
-Mungu.
-Mungu anajua kila kitu.

-Mungu alimtaka Adamu amsikilize.
-Mungu anawataka watu wote wamsikilize.

-Ukweli wa Mungu uko kwenye Bibilia.

-Mungu anawataka watu wote wasikilize yale yote yameandikwa kwa Biblia.